

Sababu za kufanyika Uchaguzi Mdogo

Uchaguzi Mdogo hufanyika kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura 292 na kifungu cha 37 (3) na 113 cha sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na ibara ya 71 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sababu hizo ni pamoja na;

- Diwani au Mbunge Kufariki au kujiuzulu
- Diwani au Mbunge kukosa sifa ya kuendelea na nafasi yake kwa mujibu wa sheria
- Matokeo kupingwa mahakamani na mahakama kutoa hukumu ya kubatilishwa kwa matokeo hayo.
- Diwani au Mbunge kujitoa, kuvuliwa au kubadilisha Uanachama katika Chama kilichompa dhamana mgombea ya kugombea

Idadi ya Chaguzi Ndogo zilizofanyika na Miaka yake.

1) Baada ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa mwaka 1995 Tume iliendesha chaguzi ndogo za ubunge ishirini na moja (21) katika majimbo ya uchaguzi ya Temeke, Magu, Morogoro Kaskazini, Ludewa, Makete, Muleba kusini, Arusha, Singida Kaskazini, Kahama, Kishapu, Sengerema, Mikunguni, Ulanga mashariki, Bunda, Mitema, Ubungo, Bukoba vijijini, Nyangwale, Kigoma na Kibaha.

Uchaguzi mdogo mmoja ulisababishwa na Mbunge kujiuzulu. Uchaguzi mdogo mwingine ulisababishwa na Mbunge mmoja kubadilisha Chama cha siasa. Chaguzi Tisa (9) zilifanywa kwasababu wabunge walifariki dunia na Chaguzi kumi (10) baada ya matokeo ya Uchaguzi mkuu kubatilishwa kwa amri ya mahakama.

2) Tarehe 22 Januari, 2017, Tume iliratibu na kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Dimani, Zanzibar na Madiwani katika Kata 20 za Tanzania Bara ambazo ni Misugusugu, Maguu, Kasansa, Ngarenanyuki, Kahumulo, Ng'hambi, Duru, Kijichi, Igombavanu, Mateves, Kiwanja cha

Ndege, Lembeni, Isagehe, Nkome, Malya, Kimwani, Ikweha, Tanga na Kinampundu.

Aidha zipo chaguzi ndogo zilizofanyika kutokana na chaguzi hizo kufutwa na kutakiwa kurudiwa kutokana na sababu mbalimbali miongoni mwa chaguzi hizo ni pamoja na zifuatazo;

- 3) Tarehe 30 Oktoba 1995, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza kufuta uchaguzi katika majimbo yote ya Mkoa wa Dar es Salaam yaani Ilala, Ukonga, Kinondoni, Ubungo, Kawe, Temeke na Kigamboni. Uchaguzi wa Marudio ulifanyika tarehe 19 Novemba 1995.
- 4) Katika Uchaguzi wa Oktoba 2000, Tume ililazimika kupanga tarehe nyingine za uteuzi na siku nyingine za upigaji kura kwa baadhi ya majimbo na kata. kutokana na vifo vya wagombea Ubunge na Udiwani, ukiukwaji wa taratibu za uteuzi, upungufu wa karatasi za kura pamoja na makosa katika uchapishaji wa karatasi za kura kwa baadhi ya majimbo ya uchaguzi na Kata. Kwa Uchaguzi wa Ubunge majimbo yaliyohusika kurudia Uchaguzi ni jimbo la Solwa, Dodoma Mjini, Kwela na Chaani kutokana na sababu za vifo na ukiukwaji wa taratibu za Uteuzi.

Kwa upande wa Udiwani Kata zilizohusika ni Pasua (Manispaa ya Moshi) Ilonga (Ulanga) Kilimanihewa (Nachingwea) Ikwiriri (Rufiji) Igowole (Mufindi) Kihorogota (Iringa)